

BENKI KUU YA TANZANIA
16 Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2303
40184 DODOMA
TANZANIA

Simu: +255 26 2962586

Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz



BANK OF TANZANIA
16 Jakaya Kikwete Road
P.O. Box 2303
40184 DODOMA
TANZANIA

Phone: +255 26 2962586

Email: botcommunications@bot.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

ORODHA YA WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA WA DARAJA LA PILI

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kutoa orodha ya watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili waliosajiliwa hadi kufikia tarehe 31 Mei 2021. Orodha hii inatolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 55(a) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 57 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili ambao hawakuwa wamewasilisha maombi ya leseni Benki Kuu kabla ya tarehe 30 Aprili 2021 hawapaswi kuendelea kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha hadi wawe wamepata leseni. Kuendelea kufanya biashara bila kuwa na leseni ya Benki Kuu ni uvunjifu wa Sheria unaoweza kupelekea faini au kifungo kwa mujibu wa Kifungu cha 16 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018.

Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutoa machapisho ya orodha iliyohuishwa ya watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili waliosajiliwa, ikiwemo orodha ya watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la tatu na la nne.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na: Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, S.L.P. 2939, Dar es Salaam au wasilisha barua pepe kwa jwsabi@bot.go.tz; vctarimu@bot.go.tz; nfmongateko@bot.go.tz; na dasasya@bot.go.tz

GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA

24 Juni 2021